

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Mtaa wa Nyanza,
S. L.P. 38

Anwani ya simu: "UCHUNGUZI"
Simu: 028-2520004
Nukushi: (028) 2520040
Baruapepe: rbcgeita@pccb.go.tz

www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

JUNI 29, 2020

**DIWANI NA WENZAKE WAWILI WAFIKISHWA MAHAKAMANI
KWA KOSA LA RUSHWA NA KUGHUSHI**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Wilaya ya Nyang'hwale Mkoa wa Geita – JUNI 29, 2020 imemfikisha Mahakamani Diwani wa Kata ya Nyampande Wilaya ya Sengerema **GEORGE KAZUNGU JOHN** na Wenzake wawili ambao ni **Hamis Msekela Maluka (Aliyekuwa Afisa Mtendaji wa Kata ya Izunya)** na **Dickson Tekele Mujungu (Afisa Elimu Kata ya Izunya)** kwa Makosa Mawili ya Kuahidi na Kupokea hongo Kinyume na **Kifungu cha 15(1)(a) na (2)** cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 na Makosa matano ya Kughushi Kinyume na **Kifungu cha 333, 335 (a) na 337** cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa mabadiliko ya mwaka 2019 na Kesi iliyofunguliwa dhidi yao ni Jinai Namba 223/2020.

Akisoma Mashitaka mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Geita **Mh Samwel Lukaja Maweda**, Mwendesha Mashitaka wa TAKUKURU Kelvin Murusuri alisema kati ya tarehe 14/12/2017 na 20/02/2020 Mshitakiwa George Kazungu John akiwa Diwani alighushi saini na mwandiko wa Marco Manoti Lubunga akidai kuwa amesambaza vifaa vya ujenzi katika Shule ya Sekondari Izunya na kuwasilisha nyaraka za uongo kwa lengo la kujipatia manufaa kiasi cha shilingi 11,428,000/=

Mwendesha Mashitaka aliieleza Mahakama pia kuwa katika kipindi hicho cha kati ya tarehe 14/12/2017 na tarehe 20/02/2020 mshitakiwa aliahidi hongo kwa washtakiwa Dickson Tekele Mujungu na Hamis Msekela Maluka ambao walipokea hongo hiyo ili kumsaidia kufanikisha malipo hayo kupitia jina la Marco Manoti Lubunga hali akijua hakustahili.

Mkuu wa **TAKUKURU** Mkoa wa Geita

Leonidas R. Felix anatoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Geita kuendelea kutoa taarifa mbalimbali za vitendo vya Rushwa na ubadhirifu katika miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na vitendo vinavyofanyika kwenye maeneo na idara mbalimbali za Serikali, Serikali za Mitaa na Halmashauri ili watuhumiwa waweze kuchukuliwa hatua za kisheria ili kukomesha vitendo vya Rushwa.

Imetolewa na

Leonidas R. Felix –Mkuu wa TAKUKURU (M) Geita